# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 2

# 62 Daudi anaacha kuua Sauli

### Kwa Biblia
1 Samweli milango 24 na 26

### Kiini cha somo
Kuonyesha kwamba tunatakiwa tuamini Mungu hata kama tunashida kubwa

### Somo


Sauli alikuwa anajaribu kuua Daudi. Daudi aliendelea kuenda akijificha. Daudi alikuwa na kikundi cha watu waaminifu waliokaa naye. Daudi na watu wake walijificha jangwani kwa msitu na kwa mapango. Wapelelezi wa Sauli waliwafwata wakijua penye wamejificha.

Siku moja Daudi na watu wake walisafiri kwenda milimani kando ya jangwa. Ilipofika jioni walipata pango na wakajificha ndani. Asubuhi yake walichunguza hilo pango. Lilikuwa pango kubwa. Lilikuwa na vipango vingine vidogo vinaelekea nje. Daudi aliamua kwamba hapo patakuwa pahali pazuri pa kujificha. Daudi na watu wake walikaa hapo kwa muda.

Wapelelezi wa Sauli walisikia kwamba Daudi alikuwa amejificha kwa milima kando ya jangwa. Wapelelezi waliambia Sauli. Sauli na askari wake walienda milimani kushika Daudi na wamuue.

## Maswali
1. Daudi alijificha wapi milimani?
2. Nani alikuwa anataka kumua Daudi?
3. Nani alikuja kupumzika pangoni?
4. Watu wa Daudi walimwambia Daudi afanye nini?
5. Mbona Daudi hakumuua Sauli?
6. Daudi alifanyaje Sauli?
7. Daudi alikuwa amejificha wapi mara ya pili?
8. Daudi alipoenda kwa kambi ya Sauli, mtu wake alimwambia afanye nini?
9. Mbona Daudi hakuua Sauli?
10. Daudi alichukua nini kutoka kwa kambi ya Sauli?

## Majibu
1. Daudi alijificha ndani ya pango.
2. Sauli alikuwa anataka kumuua Daudi.
3. Sauli alikuja kwa pango kupumzika.
4. Watu wa Daudi walimwambia aue Sauli.
5. Daudi hangeua Sauli kwa sababu alikuwa ametiwa mafuta na Mungu kuwa Mfalme.
6. Daudi alikata kipande cha vazi la Sauli.
7. Daudi alikuwa amejificha nyikani.
8. Mtu wa Daudi alitaka aue Sauli.
9. Daudi hangeua Sauli kwa sababu alikuwa ametiwa mafuta na Mungu kuwa Mfalme.
10. Daudi alichukua mkuki wa Sauli na kopo lake la maji.

Mtu mmoja wa Daudi alikuwa akikesha akiangalia maadui. Aliona Sauli na askari wake wanakuja. Alihadharisha Daudi. Daudi na watu wake walijificha ndani ya pango ndogo nyuma ya pango kubwa.

Sauli na askari wake walitafuta kila mahali milimani. Baadaye wakaja kwa pango lenye Daudi alijificha na watu wake. Sauli na watu wake walikuwa wamechoka. Sauli alienda ndani ya pango na kulala ili apumzike.



Sauli hakujua kwamba Daudi na watu wake walikuwa wamejificha mwisho wa lile pango kubwa. Sauli alilala chini kupumzika. Watu wa Daudi walimwambia, "Ua Mfalme Sauli. Mungu amekuwekea mikononi mwako." Lakini Daudi hangeweza kuua Mfalme Sauli. Sauli alikuwa ametiwa mafuta ya ufalme kwa jina la Bwana Mungu. Daudi hangeweza kuua Mfalme aliyetiwa mafuta na Mungu. Daudi aliamini kwamba Mungu atamfanya Mfalme kwa wakati wake. Mungu alikuwa ameahidi kwamba Daudi atakuwa Mfalme baadaye. Daudi aliamini kwamba Mungu atatimiza ahadi yake.

Daudi alinyemelea pole pole mpaka alikolala Sauli. Daudi alikata upindo wa vazi la Sauli. Hii inadhihirisha kwamba angeua Sauli alipokuwa akilala, lakini hakumua.

Sauli na watu wake walimaliza kupumzika. Waliondoka kwenda kutafuta Daudi. Walipoenda hatua kidogo, Daudi alipaza sauti, "Bwana wangu, Mfalme! Mbona unataka kuniua? Sitakudhuru. Nilikuwa nimejificha nyuma ya pango wakati ulilala. Ningekuua. Watu wangu walitaka nikuue lakini nikakuacha. Nilikuacha mzima."

Sauli aliangalia upindo wa vazi lake na akaona kipande kimekatwa. Aliaibika na kusema, "Daudi, ni wewe? Wewe ni wa haki. Nimejaribu kukuua lakini umekuwa mzuri kwangu, na kuokoa uhai wangu. Sitajaribu kukuua tena."

Sauli alirudi nyumbani na akaacha Daudi kwa amani. Lakini hakuchukua muda kukadhabika. Wivu wake ulirejea tena. Alitaka kumuua Daudi. Alituma wapelelezi kuchunguza alipojificha Daudi.

Daudi alikuwa amejificha nyikani. Sauli na askari wake walienda kumtafuta. Walipiga kambi katika vilima vilivyo karibu na hiyo nyika.

Watu wa Daudi walikaa wakiwa waangalifu kuhuzu Sauli. Walijua penye Sauli na askari wake walikuwa wamepiga kambi. Usiku moja Daudi alienda kwa kambi. Daudi na mmoja wa watu wake walienda pole pole mpaka kwa kambi ya Sauli. Walipata Sauli analala. Sauli alikuwa amelala na mkuki wake umechomwa chini karibu na kichwa chake. Askari wake walikuwa wamemzunguka na wamelala. Mtu aliyekuwa na Daudi alitaka kumuua Sauli. Lakini Daudi alisema, "Siwezi kuua Mfalme aliyetiwa mafuta na Mungu. Nitaamini kwa Mungu. Atatimiza ahadi zake."

Daudi alichukua mkuki wa Sauli na kopo lake la maji karibu na kichwa cha Sauli. Halafu Daudi na mtu wake wakaondoka pole pole.

Daudi na watu wake walivuka ponde na kuenda kwa kilima kingine. Daudi alipaza sauti kutoka huko akiwambia askari wa Sauli. "Mbona hamwezi kulinda Mfalme? Mtu alikuja kuua Mfalme jana usiku na nyinyi hamkumzuia. Wapi mkuki na kopo la maji ya Sauli."

Pale Sauli alitambua sauti ya Daudi. Akauliza, "Daudi, hiyo ni sauti yako? Daudi alimuuliza, "Mbona unanifukuza? Nimekukosea nini? Usiku wa jana ningekuua. Lakini nilikuacha mzima."

Halafu Sauli akaibika. Akasema, "Sitajaribu kukuua tena kwa sababu hukuniua jana usiku." Sauli alirudi nyumbani na kuacha Daudi na watu wake kwa amani.

